

UYOGAPLUS

MAANDALIZI YA KIMENGENYWA

MAJANI

Majani yawe makavu

Katakata majani urefu wa inch² hadi inch³.

Pima uzito wa majani makavu baada ya kuya katakata.

Loweka majani ndani ya maji kwa kipindi cha masaa 24.

Anika majani ya toe maji.

Changanya chokaa asilimia 1% ya uzito wa majani makavu.

MFANO: kimengenywa cha uzito wa 100kg

kilo 99kg ziwe za majani

kilo 1kg iwe ya chokaa



MARANDA (SAWDUST)

Maranda mazuri ni yale ya mti mgumu yapo kama vumbi (yasiwe makubwa sana).

Matumizi ya Maranda katika kilimo cha uyoga ni sawa na matumizi ya majani, lakini katika kutumia Maranda unashauriwa kuchanganya na vimenegenywa(virutubisho),vingine kama majani, sukari, samadi, na pumba kuongeza uzalishaji.

Maranda hulowekwa kwa kipindi cha siku saba na kuvundikwa kwa kipindi cha siku 7 baada ya kuchanganywa na virutubisho.



Mchanganyo wa Maranda na Majani.

Asilimia 70% Maranda, asilimia 26% majani (mpunga au mgomba), 1% pumba za mahindi, 1% sukari, 1% samadi na 1% chokaa.

MFANO: Kimengenywa cha uzito wa 1000kg

700kg ni Maranda

260kg ni majani

10kg pumba

10kg sukari

10kg samadi

10kg chokaa



Mchanganyo wa Maranda na pumba za mpunga.

70% Maranda-----700kg

27% Pumba-----270kg

1% Sukari-----10kg

1% Samadi-----10kg

1% Chokaa-----10kg



Kujaza mifuko/viriba

Mifuko inayofaa Zaidi ni ile ya ukubwa wa inch 8 kwa 16, iwe na rangi nyeupe.

Mifuko hua ipo wazi pande zote mbili tumia kamba ya katani kufanga upande mmoja.

Jaza kimengenywa chako kwa kushindilia huku ukiwa makini usitoboe mfuko na ufunge mfuko wako.



Kutakasa kimenegenywa(chems ha)

Baada ya kujaza kimengenywa ndani ya mifuki, chemsha mifuko yenyeye kimengenywa kwa kutumia pipa kwa mda usio pungua masaa4 na kuendelea.

Badaa ya masaa4 opoa mifuko iweke ndani ya chumba kisafi ipoe kwa kipindi cha masaa 24.

